


# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com




## MATANGAZO: DOMINIKA YA 4 YA MWAKA A - 01.02.2026

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA 01.02.2026 | **DOMINIKA YA 4 YA MWAKA A**<br>**HITIMISHO MCHANGO WA MAENDELEO MWEZI JANUARI 2026**<br>**DOMINIKA YA ZAKA**<br>Michango yote ni kwa ajili ya **Tumaini Media** |
| 2. | JUMATATU 02.02.2026 | Sikukuu ya kutolewa Bwana Hekaluni - Baraka ya Mishumaa na Siku ya Sala kwa Maisha ya Wakfu. |
| 3. | JUMANNE 03.02.2026 | Siku ya kutoa Baraka ya shingo |
| 4. | JUMAMOSI 07.02.2026 | Jumamosi ijayo 07.02.2026 kutakuwa na Misa katika JNNK Mt. Timotheo kwa ajili ya heshima ya Msimamizi wao saa 1:00 asubuhi.<br><br>Pia ni Jumamosi ya kwanza ya mwezi - Misa kwa heshima ya Moyo Safi wa Mama Maria - Misa Parokiani saa 11:00 alifajiri. |
| 5. | DOMINIKA 08.02.2026 | **DOMINIKA YA 5 YA MWAKA A**<br><br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Kristo Mfalme<br>Watangaza Neno:Juliana Kisimbi na Afred Ngowi<br><br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Monica<br>Watangaza Neno:Angela Kingu na Scolastika Mwenda<br><br>**Misa ya 3: Watoto**<br>Wasimamizi: Kristo Mfalme na Mt. Monica<br><br>**Mchango wa 2 ni kwa ajili ya ujenzi** |
| 6. | UHAKIKI WA WALIOSAJILIWA KWA ZAKA | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kufuatilia bahasha walizochukua kwa ajili ya uhakiki wa wasajiliwa wa Zaka. Zaka ya mwezi Januari wote tutatumia bahasha hata kama umelipia benki weka slipu katika bahasha, andika jina, simu, Jumuiya na namba ya zaka kama umesajiliwa. Bahasha zote zirudishwe Dominika ya leo 01.02.2026 |
| 7. | MKUTANO WA HALMASHAURI YA WALEI PAROKIA | Kutakuwa na Mkutano wa Halmashauri ya Walei Parokia Dominika ijayo tarehe 08.02.2026 mara baada ya Misa ya kwanza. Wahusika ni viongozi wa Kamati Tendaji za Jumuiya zote na Wenyeviti wa Vyama |

| | | |
|---|---|---|
| | | vya Kitume Parokia. Viongozi wote waliochaguliwa wakiwepo wa kujaza mapengo ambao hawajaapa wataapishwa katika Misa ya Kwanza na baadaye kushiriki mkutano wa H/W Parokia. |
| 8. | SENSA YA WAAMINI 2025/2026 | Tunazishukuru Jumuiya zote kwa kukamilisha zoezi la Sensa ya waamini. Tunaowajibu wa kuwahamasisha wale wote ambao wanaishi bila Sakramenti kuhakikisha wanapata Sakramenti husika. |
| 9. | CHAGUZI ZA KUJAZA MAPENGO KATIKA JUMUIYA NA KANDA | Jumamosi ijayo 07.02.2026 utafanyika uchaguzi wa kujaza mapengo ya viongozi wa Kamati Tendaji Jumuiya katika Jumuiya ya Mt. Yohane Mtume na Mwinjili |
| 10. | HUDUMA KATIKA OFISI YA MAPADRE | Wiki nzima hakutakuwa na huduma ofisini kwani mapadre wote watakuwa kwenye mkutano kwa wiki nzima. |
| 11. | WAWATA | Leo kutakuwa na Mkutano wa viongozi wa WAWATA wa Jumuiya zote mara baada ya Misa ya kwanza. |
| 12. | WATANGAZA NENO | Watangaza Neno wote wanaopangwa kutangaza Dominika wanatakiwa kufika Parokiani jioni ya Jumamosi husika kwa ajili ya mazoezi, ambao hawataweza kuhudumu kwa sababu za msingi watoe taarifa mapema. |
| 13. | KONGAMANO LA UTOTO MTAKATIFU TAIFA | Baraza la Maaskofu limeandaa Kongamano la Utoto Mtakatifu kitaifa jimboni Kigoma, 18-22 Juni, **Kauli mbiu**: **Kujifunza, kujitambua – Utoto Mtakatifu na Umisionari**. Gharama ya ushiriki kila mmoja Shs. 315,000/=. Mwisho wa kulipia ni tarehe 31.03.2026. |
| 14. | VIJANA | Vijana watakuwa na kikao Dominika ya 15.02.2026 mara baada ya Misa ya pili. Vijana wote wanaalikwa kushiriki. |
| 15. | AHADI ZA MAVUNO | Wale wote walioahidi mavuno na hawajakamilisha wanakumbushwa kukamilisha ahadi hizo kabla ya mwisho wa Januari yaani jana 31.01.2026. |
| 16. | MCHANGO WA MAENDELEO | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuwasilisha maoni ya wanajumuiya kuhusu kuendelea na mchango wa maendeleo au kubakiza na kuhimiza zaka peke yake. Tukumbuke mwisho wa kuwasilisha maoni ya wanajumuiya ilikuwa ni jana 31.01.2026. |
| 17. | UWASILISHAJI WA BARUA NA TAARIFA OFISINI | Uandikaji wa taarifa au barua zinazokuja ofisi ya Halmashauri ya Walei au Paroko zisainiwe na viongozi wawili na mhuri husika. Ziwasilishwe nakala mbili, moja inabaki ofisini na ya pili itagongwa mhuri na kurejeshewa wawasilishaji kwa kumbukumbu. |
| 18. | BAHASHA ZA PMS | Ofisi ya PMS Taifa inawakumbusha waamini wote ambao walichukua Bahasha za PMS na hawajazirudisha kuzirejesha. Kuanzia Jumatatu - 02.02.2026 mwakilishi wa PMS atapita kuzikusanya. |
| 19. | MKESHA WA SHUKURANI | Kutakuwa na mkesha wa Shukrani hapa Parokiani Ijumaa ya Kwanza ya mwezi 06.02.2026 kuamkia Jumamosi ya Kwanza ya mwezi 07.02.2026 itakapoadhimishwa Misa kwa Heshima ya Moyo Safi wa Maria. Mkesha utaanza SAA 4:00 usiku. Wote tunakaribishwa |

| | | |
|---|---|---|
| 20. | VMJ NA KANDA | VMJ na Kanda wahakikishe wanawasilisha taarifa na mipango/kalenda zao za 2026 leo Dominika ili ziweze kujumuishwa katika Kalenda Kuu ya 2026 kwa Mkutano wa Halmashauri. |
| 21. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kanisa la Kisinodi….. Ushirika, Ushiriki na Umisionari***

**TANGAZO LA USHEMASI KWA MARA YA KWANZA**

Mhashamu Askofu Mkuu Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFMCap wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam anatangaza Daraja ya Ushemasi wa Mtawa Richard Seraphine Mlay wa Shirika la Mateso ya Yesu Kristo (Passionist Fathers) anatarajia kupewa Daraja Takatifu ya Ushemasi tarehe 28.02.2026 huko Rio de Jeneiro nchini Brazil. Tumuombee ili aweze kufikia Daraja hiyo anayoitamani.

**MASOMO YA DOMINIKA – DOMINIKA YA 5 YA MWAKA A – 08.02.2026**

| | |
|---|---|
| SOMO I | Isa. 58: 7-10 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 112:4-9 |
| SOMO II | 1Kor 2:1-5 |
| SHANGILIO | Mdo.16:14 |
| INJILI | Mt 5:13-16 |